**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

**"KIZIDUO"**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 21 OKTOBA, 2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI**

## 1.0 WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Wilfred L. Sumari | - Diwani Kata ya Chanzuru | - Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Kisena M. Mabuba | - Mkurugenzi Mtendaji Wilaya | - Katibu |
| 3. | Mhe. Vicent E. Lusinde | - Diwani Kata ya Zombo | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Shani K. Baraza | - Diwani Kata ya Kidete | - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Meshack I. Munyi | - Diwani Kata ya Uleling'ombe | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Hussein H. Mwinchea | - Diwani Kata ya Mkwatani | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zuhura R. Kindunda | - Diwani Viti Maalum Tindiga | - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Subiri J. Mwamalili | - Diwani Kata ya Rudewa | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Godian W. Makoye | - Diwani Kata ya Vidunda | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Salum A. Mponzi | - Diwani Kata ya Ruhembe | - Mjumbe |

## 2.0 WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Palamagamba I. Kabudi (Mb) | - Mbunge Jimbo la Kilosa | - Kwa taarif |
| 2. | Mhe. Dennis Londo (Mb) | - Mbunge Jimbo la Mikumi | - Kwa taarif |

## 3.0 WATAALAMU WALIOHUDHURIA.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Merick Ngoko | - Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala Wilaya |
| 2. | Cheyo P. Nkelege | - Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili Wilaya |
| 3. | Oswald Mwakalasi | - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara Wilaya |
| 4. | Exavery Luyagaza | - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji Wilaya |
| 5. | Mwl. Zakia Fandey | - Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi Wilaya |
| 6. | Kanuda Erasto | - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia, Habari na Mawasiliano Wilaya |
| 7. | Neema Mwinyipembe | - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi Wilaya |
| 8. | Mwl. Richard Mkwai | - Kaimu Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu |
| 9. | Elina D. Dastan | - Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Wilaya |
| 10. | Aloyce O. Semiono | - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa taka ngumu Wilaya |
| 11. | Nyabahwela Mahuyu | - Kaimu Mganga Mkuu Wilaya |
| 12. | Rwegerela T. Katabaro | - Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Wilaya |
| 13. | Makugila S. Eliuta | - Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani Wilaya |
| 14. | Mwl. Sebastian Msuya | - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari Wilaya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15. | Gladys Mapeka | - | Afisa Habari |
| 16. | Mwl. Omari N. Jaka | - | Afisa Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Mikumi |
| 17. | Dk. Yuda L. Mgeni | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi Wilaya |
| 18. | Diana Mahimbali | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki Wilaya |
| 19. | Idrisa R. Jukulu | - | Afisa Biashara |
| 20. | Mathayo S. Rumas | - | Afisa Mapato |
| 21. | Regnald G. Simba | - | Afisa Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Kilosa |

**4.0 WAALIKWA.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Sara D. Balula | - | Afisa Tarafa Kilosa Mjini |
| 2. | Mwl. Mary Kahumbi | - | Mthibiti Ubora Elimu |
| 3. | Halima B. Nyange | - | Afisa Tarafa Ulaya |
| 4. | Geofrey Mwihumbo | | Afisa Tarafa Mikumi |
| 5. | Job A. Mchalo | - | Afisa Tarafa Kidete |
| 6. | Sabina Sugwa | - | Afisa Tarafa Kimamba |
| 7. | Moses M. Nchimbi | - | Afisa Tarafa Magole |
| 8. | Mrisho A. Mrisho | - | Mwenyekiti Mamlaka ya Mji Mdogo Mikumi |
| 9. | Hussein Fadhili | - | Mwenyekiti Mamlaka ya Mji Mdogo Kilosa |

**5.0 SEKRETARIETI.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Nyamate L. Muya | - | Mwandishi wa Mikutano |
| 2. | Leo M. Msigala | - | Mwandishi wa Mikutano |

**MUHT.NA. 22/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 07:33 Mchana kwa kuwakaribisha na kuwasalimia wajumbe waliohudhuria.

**MUHT.NA. 23 /2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA.**

Agenda 14 zilithibitishwa zitumike kwenye kikao.

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Kawaida Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 16 na 17 Septemba, 2021 na muhtasari maalum wa tarehe 27 Septemba, 2021.
4. Yatokanayo na Muhtasari wa Kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha Uongozi na Mipango tarehe 16 Septemba, 2021.
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022.
6. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha kwanza Julai – Septemba, 2021/2022.
7. Taarifa ya Ukaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022.

8. Taarifa ya Kitengo cha Manunuzi kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022.
9. Maombi ya kubadili matumizi ya bajeti katika baadhi ya miradi kwa bajeti ya mwaka, 2021/2022.
10. Eneo la ujenzi wa Ukumbi wa Halmashauriya Wilaya ya Kilosa.
11. **Taarifa ya Mapokezi ya Fedha.**
12. Taarifa mbalimbali kutoka kwaMkurugenzi Mtendaji.
    i.) Taarifa ya Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022.
    ii.) Kazi zilizotekelezwa na Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021,2022.
    iii.) Taarifa ya Kitengo cha Sheria kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022.
    iv.) Taarifa ya utekelezaji wa kazi za kawaida kitengo cha TEHAMA kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022.
    v.) Taarifa ya utekelezaji ya mpango wa kunusuru Kaya Masikini kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022.
    vi.) Mabadiliko ya Watia saini kwenye Akaunti za Halmashauri.
    vii.) Taarifa ya vifo vilivyotokea katika kipindi cha mwezi Septemba, 2021 katika Vituo vya kutolea huduma za Afya Wilayani.
13. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
14. KufungaKikao.

**MUHT NA. 32/2021/2022: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA.**

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa kuwa, Halmashauri imepokea fedha kupitia mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Fedha hizo ziko nje ya bajeti ya 2021/2022 kiasi cha Sh. 4,330,000,000.00, fedha hizi ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali za maendeleo katika maeneo yaliyoainishwa hapo chini.

i.) Ujenzi wa madarasa 147 – Elimu Sekondari 2,940,000,000.00.
ii.) Ujenzi wa madarasa 39 – Elimu Msingi 780,000,000.00.
iii.) Ujenzi wa nyumba ya mtumishi – Hospitali ya Wilaya Sh. 90,000,000.00.
iv.) Ununuzi wa mashine ya X – ray Sh. 420,000,000.00
v.) Ujenzi wa ICU katika hospitali ya Wilaya Sh. 100,000,000.00

Jumla ni Sh. 4,330,000,000.00.

Aidha, mchanganuo wa maeneo hayo miradi hii itatekelezwa kama ulivyooneshwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwenye Sekta za Elimu Msingi na Sekondari.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa.

1. Unatakiwa upatikane ufafanuzi wa matumizi ya fedha hizi.
   - Miradi itatekelezwa kwa kutumia mpango wa Haliki "Force Account", hadi tarehe 15 Desemba, 2021 inatakiwa miradi iwe imekamilika.
2. Kuhusu matumizi ya nguvu za wananchi katika utekelezaji miradi hii ya ujenzi wa madarasa.

- Matumizi ya nguvu za wananchi kwa kuhamasika wenyewe yanakubalika lakini maelekezo ni kuwa wananchi wasichangishwe.

3. Gharama ya kujenga darasa hutofautiana kutoka eneo moja na eneo lingine, unatakiwa umakini.
   - Kunatakiwa kuwe na uwazi katika matumizi ya fedha hizi, matumizi ya ramani iliyotolewa.

Taarifa ilipitishwa.

**MUHT.NA. 35/2021/2022: KUFUNGA KIKAO.**
Mwenyekiti alifunga kikao saa 11:30 Jioni kwa kuwashukuru wajumbe waliohudhuria na kufanikisha kikao.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA:**

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| MKURUGENZI MTENDAJI (W) KILOSA | MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA (W) KILOSA |

**TAREHE** 10/06/2022